SOMO LA KWANZA



YESU KRISTO NI NANI?

Tafadhali andika jina lako hapo juu kisha jaza nukuu za Biblia katika nafasi zilizotolewa.

ATU WENGINE WANASEMA NINI JUU YAKE

Fikiria wewe mwenyewe umeingia kwenye ndege/usafiri wa anga ukisafiri, sio kwenda nchi nyingine, bali kurudi nyuma mpaka nyakati zilizopita! Ghafla ukatua katika nchi ya Israeli kama ilivyokuwa miaka 2,000 iliyopita. Unapotoka nje ya ndege unagundua kuwa kila mmoja anaongea/anaongelea mwanamume/mtu mmoja aitwaye Yesu, kutoka mji uitwao Nazareti. Baadhi ya watu wanampenda, bali wengine wanamchukia. Baadhi wakinung'unika na kusema kuwa yeye ni mleta fujo au mvurugaji na mdanganyifu,[1] na wengine wanamsema kuwa ni mtu mwema tena maalum kutoka kwe Mungu, nabii. Na wapo baadhi wanoamini kuwa Yeye ni mwana wa Mungu, Kristo.

Rudi katika nyakati za nyuma

Unapowasikiliza, kwa uhakika unapatwa na mshangao ni kwa jinsi gani Yeye anaweza kuamsha hisia zenye nguvu ya chuki kwa baadhi, na kwa wakati uo huo kuwapata wengine ambao wanapenda ibada na hata wanaabudu kinyume na wengine. Jambo moja ni wazi unapomtazama mwenyewe. Huyu ni mtu ambaye kwa hakika anajali, muwazi na jasiri!

Katika somo hili tutaangalia zaidi yale watu waliyoyasema juu ya Yesu, na kile Yesu alichokisema juu yake mwenyewe.

MATAKWA YA MAKUSANYIKO (WATU)

Alikusanya makundi makubwa

Idadi ya wengi walikusanyika kumsikiliza Yesu na kuponywa.
Angalia katika Luka 5:15

.....

.....

.....

.....

MAONI YA BAADHI

Kwa mitazamo tofauti tofauti juu ya Yesu soma Mathayo 16:13-16.
Andika mstari wa 16

.....

.....

Ukumbusho wa kihistoria:
Maisha ya Kristo duniani yalianza katika siku za utawala wa Kaisaria Agusto wa Roma (27 KK- 14 BK)

Kwa tabia za watu wengine angalia nukuu hapo chini namba. [2]

[1] Yohana 7:12

[2] Tabia kinyume (Yohana 7:12); Ibada (Mathayo 26:7); Kuabudu (Mathayo 14:33).

ALICHOSEMA YESU JUU YAKE MWENYEWE

Kwa ushupavu/ ushujaa kama tausi

Baadhi ya watu ni kama tausi, kwa kiburi hujaribu kujiinua kwa utukufu wao binafsi. Wanapenda kujisifia ni watu wa namna gani na uwezo wao wa kutenda vitu. Wanapenda waonekane wa maana/muhimu. Tunagundua wantu wa namna hiyo ni wa jinsi gani, na hatuchukui tahathari juu yao. Ni kwa jinsi gani mtu ambaye ni mnyenyekevu na asiyethaminika kama Yesu aongee vitu vikubwa, inahitajika kuchukuliwa kwa uangalifu. Ni kwa jinsi gani mtu mnyenyekevu na asiyejithamini kama Yesu aongee vitu vikubwa juu yake mwenyewe isipokuwa, kwa hakika walikuwa wakweli? Tumeona tangu mapema juu ya yale watu wengine waliyoyasema juu ya Yesu. Hebu sasa tuone alichosema Yesu juu yake mwenyewe.

USEMI/MADAI YA YESU

Nyawezekana Yesu alikuwa punguani au alisema ukweli.

Hakuna kiongozi wa kiroho au nabii aliyewahi kujiongelea juu yake binafsi kama Yesu alivyofanya. Waliwachagua na kuwaelekeza watu kwa Mungu, lakini Yesu aliwaelekeza watu kwake Yeye binafsi. Alijitangaza mwenyewe kuwa ndiye njia ya kumwendea Mungu, na ndiye suluhisho kwa mahitaji yote ya watu. Haishangazi baadhi ya watu waliuchukulia usemi Wake kuwa kufuru na ukaidi kinyume na Mungu. Walilazimishwa kuchagua mawili, aitha wamwamini au wamlaumu kwa kumpinga!

Yesu alisema kuwa yeye ni Mkate wa Uzima, Nuru ya Ulimwengu, na Mlango wa Wokovu.[3] Pia alidai kuwa yeye ndiye Njia ya kwenda kwa Mungu. Angalia Yohana 14:6

.....

.....

.....

MADAI YA KUWA ALIKUWEPO HATA KABLA YA UUMBAJI

Kabla wakati kuanza

Yesu aliongea juu ya wakati, kabla ya ulimwengu kuumbwa, alipokuwa anaishi na Mungu. Angalia Yohana 17:5

.....

.....

.....

Alieleza kuwa alikuwepo kabla ya Ibrahimu- mtu aliyeishi muda mwingi kabla ya Yesu, kama sisi tulivyo kabla Yake.[4]

MADAI YA KUWA YEYE NI MUNGU-MTU

Mwana wa Mungu Mkuu

Kwa kumalizia, Yesu kumwita Mugu Baba Yake, Yesu alidai kuwa yeye ni Mwana wa Mungu kwa kusudi maalumu. Lilikuwa dai la kuonyesha kuwa Yeye ni sawa na Mungu. Angalia Yohana 5:18

.....

.....

.....

.....

[3] Yohana 6:35, Yohana 8:12, Yohana 10:9.

[4] Yohana 8:56-58.

MIUJIZA YA YESU ILIONYESHA NINI

Ishara zilikuwa na maana

Kila sehemu iliyotuzunguka ina ishara– na yote ina maana kwa namna Fulani. Ishara ya kulia inawaambia madereva wachukue tahadhari, maana watu wanafanya kazi barabarani. Miujiza aliyoifanya Yesu ilikuwa ishara, nazo pia zina maana. Injili ya Mathayo, Marko, Luka, na Yohana zimeorodhesha miujiza mingi na ishara nyingi alizozifanya Yesu. Miujiza mingi aliyoifanya Yesu ilikuwa yenye huruma/kujali. Aliwaponya wale waliokuwa na magonjwa, na alimhurumia kiwete akamfanya atembee na kipofu apate kuona..[5] Aliwafufua hata wafu.

Lakini pia Yesu alifanya miujuza iliyoonyesha nguvu Zake zilizo zaidi ya asili. Alitembea juu ya maji, alituliza dhoruba na akazidisha chakula kuwalisha maelfu waliokuwa na njaa. Katika tukio moja alibadilisha maji kuwa divai.

MAANA YA ISHARA ALIZOZIFANYA YESU

Miujiza ya Yesu ilikuwa ya kuthibitisha vitu alivyovisema juu Yake mwenyewe.[6] Zilikuwa ishara za kuonyesha kuwa kwa hakika Yeye ndiye aliyekuwa, katika hali ya kipekee, Mwana wa Mungu. Angalia Yohana 20:30-31

Ishara za Yesu

.....

.....

.....

.....

.....

.....

KWA NINI YESU ALITOA ISHARA

Hakuna anayeonyesha ishara ili aaminiwe.[7] Yesu alifanya miujiza ili kwamba watu wasiwe na sababu ya kuegemea kwa kutokuamini kwao. Soma Yohana 15:22-24. Andika mstari wa 24

Sasa hakuna udhuru

.....

.....

.....

.....

Miujiza Yake Yesu iliandikwa kwa faida yetu, ili kwamba nasi tusiwe na udhuru wa kutokuamini.

KUUNDA MSIMAMO WAKO BINAFSI

Pimeni matokeo

Sheria za mahakamani zina maana ya kupima kwa umakini maelezo yanayotolewa ili kubaini ukweli. Kwa usawa kama huu wa kisheria, waandishi wa Agano Jipya waliandika kwa mtiririko unaotusaidia kupima ukweli kumhusu Yesu- na hiki ndicho masomo haya yamelenga kufanya. Wewe ni hakimu, na wanafunzi wa Yesu yaani Mitume ni mashahidi. Angalia Matendo ya Mitume 2:32

.....

.....

[5] Mathayo 15:30-31.

[6] Yohana 10:25 na Matendo ya Mitume 2:22.

[7] Mathayo 12:38-39 na Yohana 20:29.

UDHIBITISHO WA ZIADA: YESU ALISAMEHE DHAMBI

Kitu cha ziada cha kupima

Umekuwa ukipima vitu alivyovisema Yesu juu yake Binafsi, na maana ya miujiza yake. Unapaswa pia ujihusishe/ujali jinsi Yesu alivyosamehe dhambi. Hakuna nabii au mwalimu wa dini aliyefanya haya (kusamehe dhambi), ni Mungu pekee awezaye kusamehe dhambi. Wengi walichukia waliposikia Yesu akimwambia mtu Dhambi zako zimesamehewa. Hii ilieleweka kuwa Yeye ni Mungu. Soma Luka 5:18-21. Andika mstari wa 20 na 21

.....

.....

.....

.....

.....

Kuona moyo

Hii pia ilieleweka kuwa Yesu angeweza kuusoma moyo wa mtu, na kujua ni lini alipokuwa na huruma ya kweli.[8]

BADO UTHIBITISHO MWINGINE: KUZAA KWA BIKIRA

Ili tuweze kupata majibu mazuri juu ya kumtafiti Yesu ni lazima tupime walichokisema waandishi wa Agano Jipya juu ya kuzaliwa Kwake. Walielezea kwa uwazi kwamba alizaliwa na bikira – mtu ambaye hajawahi kuwa na mahusiano ya kimwili (ngono) na mwanaume! Roho wa Mungu ndiye aliyeleta habari ya kuzaliwa Kwake. Soma Luka 1:26-35. Andika mtari wa 35

Je! Kuna kitu kigumu sana kwa Mungu Mkuu?

.....

.....

.....

.....

.....

Hili pia linamtenga Yesu kuwa mtu wa tofauti na watu wengine. Inapendekezwa kuwa Yeye ni zaidi na zaidi ya mwanadamu – kwamba Yeye pia ni Mungu.[9]

KWA KUMALIZIA (HITIMISHO)

Hitimisho lako ni nini? Yesu alianza kuishi kwake katika Dunia hii kwa utofauti usiolinganishwa kabisa, na aliuacha ulimwengu sawasawa na kuja kwake kusikokuwa kwa kawaida. Kifo Chake siyo hitimisho Lake. Atakuja hai na hatakufa tena.

Ukumbusho wa kihistoria: Yesu alikuwa na miaka 33 alipokufa kifo cha kuteseka sana kwa kusulubiwa. Lakini haikuwa mwisho!

Kufufuka kwa Yesu ni tukio la kihistoria, na ya muhimu zaidi ni kuwa tutajifunza somo zima linalohusu ufufuo wake baadaye.

Hivyo basi, Yesu Kristo ni nani? Alifanya maajabu yaliyowashtua watu wa siku Zake. Walitaka kujua ukweli juu Yake, kama wewe unavyotaka. Lakini kwa kumtazama mtu husika walifikia hatua ya kutoa mahitimisho tofauti tofauti.

Kama mwanachama wa mahakimu unategemewa kutoa uamuzi au hukumu yako. Utasema kama mwanafunzi Tomaso, kwamba Yeye ni Bwana wako na Mungu?[10]

[8] Kwa uthibitisho mwingine angalia Luka 7:36-50.

[9] Mathayo 1:23 (angalia neno "Mungu pamoja nasi").

[10] Yohana 20:28.